






Kimetolewa na
Ndaki ya Misitu Wanyamapori na Utalii,
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
S. L. P 3009,
Chuo Kikuu,
MOROGORO TANZANIA
Tel. Gen. Line 255 023 2603511/4 Ext. 4601
E-mail: forestry@suanet.ac.tz


CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

NDAKI YA MISITU WANYAMAPORI NA UTALII

# MKONGO

## (Afzelia quanzensis)



Family: Fabaceae (Caesalpinoideae)





## MAELEZO YA JUMLA

- Hutoa mbao zenye ubora ikifika umri wa miaka 30 - 50

## MATUMIZI (Huwa haiathiriwi na mchwa au wadudu wanaotoboa mbao)

- Chakula – majani yanaweza kutumika kama mboga, magamba na majani huliwa na tembo
- Mbao – samani, milango, mataruma ya reli, vifaa vya muziki na kutengeneza boti
- Kivuli na mapambo katika bustani
- Dawa (mizizi) – Maumivu ya kifua, figo, kichocho. Ganda huweza kutumika kama dawa ya jino linalouma



## UPATIKANAJI

- Mwinuko wa mita 300 - 1800 juu ya usawa wa bahari
- Mvua ya wastani wa 400mm – 1700mm

## MATAYARISHO YA MICHE KWA AJILI YA KUPANDA

- Ondoa mbegu kutoka katika maganda
- Mbegu huoteshwa moja kwa moja katika viriba
- Mbegu huchipua baada ya siku 10 hadi15

## UPANDAJI

- Miche

## UDONGO

- Udongo tifu-tifu na unaopitisha maji kirahisi hadi udongo wa kichachanga



## MATAYARISHO YA SEHEMU YA KUPANDA

- Shamba lifyekwe kuondoa magugu yote. Ikiwezekana lilimwe au sehemu ya kuotesha ilimmwe. mashimo yawe cm. 50
- Unyevu uwe wa kutosha kabla ya kuotesha miche

## NAFASI KATI YA MICHE

- Mita 3 kutoka mche hadi mche



